TANGAZO LA SERIKALI NA. 68 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MABADAGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Mabadaga ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipakaifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG7 yenye majira-nukta 633057MS, 9025925KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini -Mashariki katika

uelekeo wa KZ33˚42MS’ kwa umbali wa kilomita 1.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG6 yenye majira-nukta 634204MS, 9026690KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KZ13˚36MS kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG3 yenye majira-nukta 635485MS, 902700KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ52˚32MS kwa umbali wa Kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya upimaji namba MBG2 yenye majira-nukta 635777MS, 9027381KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa KZ 28˚01’MS kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG1 yenye majira-nukta 636328, 9027674KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 12˚13’MG kwa umbali wa kilomita 2.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG4 yenye majira-nukta 633887MS, 9028228KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 224˚38’KS kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG5 yenye majira-nukta 632068MS, 9026432KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea

Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 329°55’KS kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBG8 yenye majira-nukta 632686MS, 9026074KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KZ 158˚07 kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi ulipoanzia.”

Dodoma
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*